JamiiYETU

11 MSUKUMO MKALI BIMA YA AFYA KWA WOTE RUVUMA

14 MIRADI MWANZA INAONESHA UTEKELEZAJI ILANI YA CCM



Boti ya kisasa ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji iliyosaidia kuokoa watu 41 waliokuwa kwenye meli ya MV Chambo iliyowaka moto ndani ya Ziwa Nyasa ikiwa safarini eneo la Mtipwili wilayani Nyasa hivi karibuni.

Boti ya Tanzania ilivyookoa abiria wa mataifa manne Ziwa Nyasa

Na Albano Midelo

Moto ulipoanza kutanda ndani ya MV Chambo alfajiri ya Oktoba 11, 2026, hofu haikuwa tena kuhusu safari kufika mwisho wake.

Kwa abiria 44 waliokuwa ndani ya meli hiyo wakielekea Msumbiji kupitia Ziwa Nyasa, swali lilikuwa moja tu; nani angefika salama ufukweni?

Meli hiyo ilikuwa imebeba abiria wa mataifa manne ya Tanzania, Msumbiji, Malawi na Lesotho pamoja na takribani tani 10 za mzigo.

Ndani ya dakika za taharuki, safari ya kawaida ya kuvuka ziwa iligeuka kuwa operesheni ya kuokoa maisha. Watu watatu walipoteza maisha, 41 wakaokolewa.

Nyuma ya idadi hiyo, kuna simulizi nyingine muhimu zaidi. Kwamba, wakati moto ukiwaka kwenye MV Chambo, Tanzania tayari ilikuwa imeanza kujenga uwezo mpya wa kukabiliana na majanga majini.

Wiki chache kabla ya ajali hiyo, Serikali ilikuwa imezindua boti maalumu ya uokozi na kuzima moto yenye thamani ya Sh bilioni 1.5 katika Ziwa Nyasa.

Hapo ndipo tukio la MV Chambo linapogeuka kutoka kuwa taarifa ya ajali na kuwa mtihani halisi wa uwekezaji wa serikali katika usalama wa maisha ya watu.

Boti mpya yakabili 'mtihani wa kweli'

Septemba 2026, Serikali ilizindua na kukabidhi boti maalumu ya uokozi na kuzima moto yenye namba MV 009 ZT, katika eneo la Mbamba Bay, Wilaya ya Nyasa.

Kwa mujibu wa taarifa ya Serikali ya Mkoa wa Ruvuma, boti hiyo ina thamani ya Sh bilioni 1.5 na ina injini mbili zenye nguvu ya 'horsepower' 250 kwa kila moja.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Ahmed Abbas anasema uwekezaji huo ulikusudiwa kuongeza uwezo wa kukabiliana na majanga katika Ziwa Nyasa.

Hata hivyo, thamani ya boti haikuwa kwenye bei yake pekee, thamani yake kubwa zaidi imeonekana wakati ilipotakiwa kufanya ilichokusudiwa kufanya.

Hii ni kufika eneo la dharura kwa wakati na kuwezesha waokoaji kuwafikia watu waliokuwa kwenye hatari.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Ruvuma, Merania Nyabwinyo anasema boti hiyo ilisaidia kurahisisha operesheni ya uokozi na kufikisha waathirika katika huduma za afya haraka.

Kwa lugha rahisi, uwekezaji wa Sh bilioni 1.5 ulianza kupimwa si kwa ukubwa wa injini zake, bali kwa idadi ya maisha ambayo mfumo huo uliweza kuyafikia.

Abiria 44, mataifa manne na dakika za hofu

Kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya ya Nyasa, Peresi Magiri, MV Chambo ilikuwa

Inaendelea uk 13

Huduma za kifedha kidijiti zinavyobadili utamaduni wa Watanzania kuweka akiba



Chanzo: Ripoti ya Financial Sector Deepening Tanzania (FSDT) Machi 2025, Benki Kuu ya Tanzania (BoT) – Taarifa ya Mifumo ya Malipo 2025, na FinScope Tanzania 2023.

Na Mwandishi Wetu

"TOFAUTI na zamani, sasa nina sehemu nyingi za kutunza fedha zangu na ziko salama. Kuna benki, simu, hati fungani, vikoba, vyama vya ushirika vya akiba na mikopo, mifuko ya uwekezaji ya pamoja na nyinginezo."

"Si kuhifadhi fedha tu, bali pia kuwekeza kwa namna inayonipa faida. Hata fedha za jumuiya zinaweza kuwekwa sehemu mbalimbali na zikawa salama."

Mkazi wa Dar es Salaam, Eliudi Allen anatoa kauli hiyo akiakisi mabadiliko yanayoendelea katika namna Watanzania wanavyopata na kutumia huduma za kifedha.

Simu za mkononi, ambazo awali zilitumika zaidi kwa mawasiliano, sasa zimekuwa nyenzo ya kutuma na kupokea fedha, kulipia bidhaa na huduma, kuweka akiba na kupata mikopo.

Mabadiliko hayo yameongeza uchaguzi wa watumiaji wakiwamo wafanyabiashara wadogo, wafanyakazi na vikundi vya kuweka na kukopeshana.

Pamoja na urahisi unaotokana na teknolojia, bado kuna maswali kuhusu namna huduma hizo zinavyosaidia wananchi kujenga akiba ya muda mrefu, kuepuka madeni yasiyolingana na uwezo wao na kuimarisha usalama wa fedha zao.

Ripoti ya Mfumo wa Malipo ya Taifa ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ya mwaka 2025 inaonesha thamani ya miamala ya akiba za kidijiti iliongezeka kutoka Sh trilioni 1.21 mwaka 2024 hadi Sh trilioni 3.18 mwaka 2025.

Idadi ya miamala hiyo ilipanda kutoka milioni 46.47 hadi milioni 97.53, sawa na ongezeko la asilimia 110.

Takwimu hizo zinaonesha kuongezeka kwa matumizi ya mifumo ya kidijiti katika kuweka akiba, ingawa hazimaanishi moja kwa moja kuwa kila mtumiaji ana akiba ya kutosha au kwamba huduma hizo zinapatikana kwa manufaa sawa kwa wananchi wote.

Miongoni mwa mabadiliko yanayoonekana ni kuongezeka kwa huduma zinazowezesha watu kutenga fedha kupitia simu, badala ya kutegemea kutembelea matawi ya benki pekee.

Huduma hizo zinaweza kuwezesha wananchi kuweka kiasi kidogo kidogo kulingana na kipato chao, jambo linalosaidia kujenga nidhamu ya matumizi na maandalizi ya mahitaji ya baadaye.

Kwa mfanyabiashara mdogo, kutenga sehemu ya mauzo kwa ajili ya akiba kunasaidia kugharamia mahitaji ya biashara, kununua bidhaa na kukabiliana na vipindi ambavyo mapato yanapungua.

Kwa mfanyakazi, akiba inaweza kusaidia maandalizi ya ada za shule, matibabu au dharura za kifamilia.

Huduma za aina hiyo zinatolewa na watoa huduma mbalimbali, wakiwamo benki na kampuni za mawasiliano.

Miongoni mwa mifano iliyopo sokoni ni Kibubu, Kibubu Plus na Kikoba zinazopatikana kupitia Mixx by Yas.

Kibubu ni huduma ya kutenga fedha kwa ajili ya akiba kupitia simu, huku Kibubu Plus ikilenga wanaotaka kuweka fedha kwa kipindi maalumu. Kikoba, kwa upande mwingine, inalenga vikundi vinavyoweka akiba na kukopeshana.

Baadhi ya huduma hizi zinapatikana kupitia programu za simujanja na mifumo ya USSD inayotumiwa pia na simu za kawaida. Hali hiyo inaweza kusaidia kupanua upatikanaji wa huduma kwa watu wasio na simujanja au intaneti.

Hata hivyo, watumiaji wanapaswa kuelewa masharti ya kila huduma, ikiwamo namna ya kutoa fedha, ada zinazoweza kutozwa na faida inayoweza kupatikana.

Viwango vya riba au faida vinapaswa kulinganishwa kwa kuzingatia masharti halisi ya bidhaa husika.

Upanuzi wa huduma za kifedha za kidijiti umeongeza umuhimu wa ushirikiano kati ya benki na kampuni za teknolojia na mawasiliano.

Ushirikiano huo unaweza kuunganisha urahisi wa kufikia wateja kupitia simu na utaalamu wa taasisi za fedha katika kusimamia amana, mikopo na vihatarishi.

Mkuu wa Fedha na Malipo ya Kidijiti wa Mixx by Yas, Mshamma Mshamma anasema ushirikiano kati ya watoa huduma za kidijiti na taasisi za fedha unaweza kusaidia kupanua upatikanaji wa huduma mbalimbali.

Anasema teknolojia inaweza kuwezesha wateja kupata huduma kwa urahisi zaidi, huku ushirikiano na taasisi za fedha ukifungua fursa za kuunganisha malipo na huduma nyingine, zikiwamo akiba, mikopo, bima na uwekezaji.

Hata hivyo, maendeleo hayo hayamaanishi kuwa benki zinapoteza nafasi yake katika mfumo wa fedha, bali teknolojia inabadili namna benki zinavyowafikia wateja na kutoa huduma.

Mwenyekiti wa Umoja wa Mabenki Tanzania (TBA), Theobald Sabi ambaye pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, anasema teknolojia imebadilisha namna benki zinavyofanya kazi na kuhudumia wateja.

"Teknolojia haijachukua nafasi ya benki; imebadilisha namna benki zinavyofanya biashara na kuwafikia wateja kulingana na mahitaji yao. Benki zitakazofanikiwa ni zile zinazotumia teknolojia kuongeza thamani kwa wateja," anasema.



Anasema benki zinaendelea kuwekeza katika mifumo ya kidijiti, sambamba na huduma zinazotolewa kupitia matawi na mawakala.

Kwa mujibu wa Sabi, Benki ya NBC inaendelea kutumia mifumo ya NBC Kiganjani na NBC Connect, pamoja na kupanua mtandao wa mawakala na matawi.

Takwimu za BoT zinaonesha idadi ya mawakala wa benki iliongezeka kutoka 59,291 Juni 2022 hadi 189,719 Desemba 2025.

Upanuzi huo unaonesha juhudi za kupanua njia za wananchi kupata huduma za benki nje ya matawi ya kawaida.

Vikundi vya kuweka akiba na kukopeshana vimekuwa sehemu ya maisha ya kiuchumi ya wananchi wengi, hasa wale wanaotaka kuweka akiba pamoja au kupata mikopo kwa ajili ya shughuli zao.

Kwa vikundi hivyo, mifumo ya kidijiti inaweza kurahisisha kurekodi michango, kufuatilia akiba na mikopo ya wanachama na kuhifadhi taarifa za miamala.

Rekodi zinapokuwa wazi na zinapatikana kwa wanachama husika, zinaweza kusaidia kupunguza kutokuelewana kuhusu fedha za kikundi.

Hata hivyo, teknolojia peke yake haiwezi kuhakikisha uwajibikaji. Vikundi vinahitaji kuwa na kanuni zinazoeleweka, utaratibu wa kuidhinisha matumizi ya fedha, kumbukumbu sahihi na makubaliano kuhusu mikopo na marejesho.

Aidha, wanachama wanapaswa kuelewa namna taarifa zao zinavyohifadhiwa na nani anayeruhusiwa kuzifikia.

Ulinzi wa taarifa binafsi ni muhimu hasa pale huduma zinapohusisha taarifa za miamala, namba za simu na historia ya mikopo.

Pamoja na akiba, mikopo ya kidijiti imekuwa sehemu nyingine muhimu ya mabadiliko ya sekta ya fedha.

Kwa kutumia simu, baadhi ya wateja wanaweza kuomba na kupata mikopo bila kufuata taratibu zote zinazohusishwa na mikopo ya kawaida ya benki.

Kwa wafanyabiashara wadogo, mikopo hiyo inaweza kusaidia kuongeza mtaji, kununua bidhaa au kukabiliana na changamoto za muda mfupi za kifedha.

Hata hivyo, urahisi wa kupata mkopo unaweza pia kuwa chanzo cha matatizo ikiwa mkopaji hatafahamu gharama zake au uwezo wake wa kurejesha fedha.

Ripoti ya BoT ya mwaka 2025 inaonesha kuwa idadi ya miamala ya mikopo ya kidijiti iliongezeka kwa asilimia 24.98 hadi milioni 336.52, kutoka milioni 269.30 mwaka 2024.

Thamani ya mikopo hiyo iliongezeka kwa asilimia 32.29 hadi Sh trilioni 5.58 kutoka Sh trilioni 4.22 mwaka uliotangulia.

Ukuaji huo unaonyesha ukubwa wa matumizi ya mikopo ya kidijitali, lakini pia unaweka umuhimu wa elimu ya fedha na utoaji wa mikopo kwa uwajibikaji.

Kabla ya kukopa, watumiaji wanapaswa kuelewa riba, ada, adhabu za kuchelewa kulipa na muda wa marejesho. Ni muhimu pia kulinganisha gharama za huduma mbalimbali na kuhakikisha mkopo hautumiki kufidia madeni mengine bila mpango wa kuyamaliza.

Kwa upande wa watoa huduma, uwazi wa masharti, ulinzi wa taarifa binafsi na tathmini ya uwezo wa mkopaji kurejesha fedha ni muhimu ili kupunguza hatari ya madeni kupita uwezo.

Mhadhiri Mwandamizi wa Shule Kuu ya Biashara ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dk Thobias Swai anasema teknolojia imepanua upatikanaji wa huduma za malipo, mikopo, bima na uwekezaji, lakini mabadiliko hayo yanahitaji kuambatana na uelewa wa watumiaji kuhusu namna ya kusimamia fedha.

Elimu ya fedha inaweza kuwasaidia wananchi kutofautisha akiba na uwekezaji, kutathmini hatari, kupanga bajeti na kufanya maamuzi yanayolingana na malengo yao.

Kwa mfano, mtu anayetaka kuweka fedha kwa ajili ya dharura anahitaji kuzingatia upatikanaji wa fedha hizo anapozihitaji.

Anayetaka kuwekeza kwa muda mrefu, kwa upande mwingine, anapaswa kuelewa hatari, masharti na uwezekano wa kupata faida au kupata hasara.

Huduma za kifedha za kidijiti zinaendelea kupanua njia ambazo wananchi wanaweza kutumia kusimamia fedha zao.

Kuongezeka kwa matumizi ya akiba za kidijiti kunaonyesha kuwa simu zinaweza kuwa nyenzo muhimu katika kujenga tabia ya kutenga fedha kwa ajili ya mahitaji ya baadaye.

Hata hivyo, mafanikio ya sekta hiyo hayapaswi kupimwa kwa thamani ya miamala au idadi ya mikopo pekee.

Yanapaswa pia kuangaliwa kwa namna huduma hizo zinavyosaidia wananchi kujenga akiba, kupata mikopo yenye masharti yanayoeleweka, kulinda fedha zao na kuimarisha shughuli za uzalishaji.



Boti ya Tanzania ilivyookoa abiria wa mataifa manne

Inatoka 9

na abiria 44, raia 23 wa Msumbiji, 15 wa Tanzania, wanne wa Malawi na wawili wa Lesotho.

Anasema meli ilikuwa imesajiliwa Msumbiji. Ilikuwa ikisafiri kati ya Tanzania na Msumbiji na kwamba meli hiyo ilikuwa ikiwasili Tanzania kila Jumamosi na kurejea Msumbiji Jumapili.

Moto ulipotokea, changamoto haikuwa tu kuzima moto, bali kuhakikisha watu kutoka mataifa hayo manne wanaokolewa.

Mwisho wa operesheni, watu 41 waliokolewa. Watatu walifariki, akiwamo mtoto mchanga wa kike kutoka Msumbiji. Wengine ni mwanamke kutoka Malawi na Mtanzania, Yuston Chatanda.

Hii ndiyo sababu tukio hilo lina uzito zaidi ya mipaka ya Tanzania. Ziwa Nyasa si mpaka wa kisiasa pekee, bali ni eneo ambalo biashara, usafiri, uvuvi, familia na shughuli za kiuchumi huunganisha jamii za nchi mbalimbali.

Ajali moja inaweza kuwa tukio la nchi moja, lakini uokozi wake unaweza kuwa jukumu la nchi nyingi.

'Mitumbwi isingeweza kazi hiyo'

Kwa wakazi wa Mbamba Bay, usalama wa Ziwa Nyasa si mjadala wa kitaalamu unaofanyika ofisini, bali suala la maisha ya kila siku.

Mkazi mmojawapo wilayani humo, John Challe anapongeza Serikali kwa uwekezaji huo akisema, boti hiyo ya kisasa ilikuwa muhimu kuwezesha waokoaji kuwafikia manusura.

Kwa mtazamo wake, mitumbwi ya kawaida isingekuwa na uwezo sawa wa kukabiliana na tukio la aina hiyo.

Kauli hiyo inaweka wazi pengo kubwa katika usalama wa usafiri wa majini kwamba, si kila chombo kinachoweza kusafiri majini kina uwezo wa kufanya ipasavyo uokozi wa majini.

Ndiyo maana uwekezaji katika vifaa vya uokozi haupaswi kutazamwa kama matumizi ya kawaida ya serikali, bali pia kama sehemu ya mfumo wa bima ya maisha ya wananchi.

Tatizo ni sekunde za kwanza baada ya ajali

Katika usalama wa majini, tofauti kati ya manusura na waathirika mara nyingi huamuliwa na kile kinachotokea katika dakika za kwanza baada ya dharura.

Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Majini (IMO) linaweka mkazo mkubwa kwenye vifaa vya kuokoa maisha ikiwamo maboya ya kuokolea maisha, mashua na boti za uokozi, mifumo ya tahadhari na maandalizi ya dharura.

Tanzania na mfumo wa kisheria

Tanzania ina sheria na kanuni zinazosimamia usalama wa usafiri wa majini.

Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) limekuwa likisisitiza mambo ya msingi kwa waendeshaji wa vyombo.

Hayo ni pamoja na ukaguzi na usajili wa vyombo, vifaa vya kujiokolea, matumizi ya maboya, kutopakia abiria au mizigo kupita uwezo, taarifa za safari na kuangalia hali ya hewa kabla ya safari.

Hapo ndipo ajali kama ya MV Chambo inapaswa kutazamwa kama fursa ya kufanya tathmini ya mfumo mzima wa usalama.

Ziwa Nyasa na somo kutoka Ziwa Victoria

Tanzania si nchi pekee katika Afrika Mashariki inayokabili changamoto za usalama katika usafiri wa majini.

Historia ya Ziwa Victoria imeshaonesha gharama kubwa za udhaifu wa mifumo ya usalama.

Benki ya Dunia imeeleza kwamba ajali kubwa kama kuzama kwa MV Bukoba mwaka 1996 iliyohusisha vifo vingi, ilichangia kuibua kwa nguvu suala la usalama wa usafiri wa ziwani.

Mipaka inatenganisha nchi, uokozi unaunganisha

Baada ya ajali ya MV Chambo, ushirikiano kati ya Tanzania na Msumbiji ulipata sura ya vitendo.

Mkuu wa Wilaya ya Lago, Jimbo la Niassa nchini Msumbiji, Joss Achida Assane alitembelea Wilaya ya Nyasa kuanzia Oktoba 19 hadi 20, 2026 kushukuru Kamati ya Usalama ya Wilaya ya Nyasa na wananchi wa Kijiji cha Undu, Kata ya Mtipwili kwa mchango wao katika uokozi.

Assane pia akapendekeza vikao vya mara kwa mara kati ya Lago na Nyasa ili kuimarisha udhibiti wa mipaka na kukuza biashara.

Hapa ndipo ajali ilipoacha somo kubwa la diplomasia ya ujirani. Meli ilikuwa ya Msumbiji, ajali ilitokea katika maji ya Tanzania, abiria waliotoka mataifa manne. Uokozi ukawa jukumu la pamoja.

Katika mazingira kama hayo, usalama wa majini unapaswa kuangaliwa kama sehemu ya diplomasia ya mipakani na biashara ya kikanda.

Kimsingi, Dira ya Taifa ya 2050 inaweka mwelekeo wa maendeleo ya Taifa kwa miaka 25 ijayo.

Dira hiyo inalenga Tanzania yenye uchumi shindani, unaoongozwa na tija, teknolojia, ubunifu, miundombinu na huduma bora kwa wananchi.

Kwa mtazamo huo, boti ya kisasa ya uokozi Ziwa Nyasa ni zaidi ya chombo cha dharura; ni mfano wa namna teknolojia inavyoweza kuunganishwa na huduma za msingi za serikali.

Kesho ya Ziwa Nyasa haitaki boti moja pekee

Boti ya Sh bilioni 1.5 imeonesha kile ambacho uwekezaji wa Serikali unaweza kufanya unapokutana na tukio la kweli, lakini mafanikio ya muda mrefu hayatapimwa kwa idadi ya watu 41 waliookolewa katika tukio moja, bali kwa uwezo wa kuzuia ajali inayofuata.

Hapo ndipo hatua inayofuata inapaswa kuangaliwa yaani ukaguzi mkali wa vyombo, mafunzo ya mara kwa mara ya waendeshaji, maboya ya kujikolea kwa abiria wote, vifaa vya dharura, taarifa sahihi za hali ya hewa, mawasiliano ya haraka na ushirikiano wa kudumu kati ya Tanzania, Msumbiji na nchi nyingine zinazotumia Ziwa Nyasa.



Viongozi kutoka Wilaya ya Lago nchini Msumbiji wakiwa na wenzao wa Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma.